



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA**



HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

Taf. Unapojibu nakili

KUMB Na. KDC/L.20/VOL.XIX/10

Tarehe: 12/10/2023

Mkurugenzi Mkuu
Kituo cha Uwekezaji
Mtaa wa Shabaan Robert
S.L.P 938
DAR ES SALAAM



**YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA IDEAL DETONATORS TANZANIA KWA
AJILI YA UWEKEZAJI ENEO LENYE UKUBWA WA EKARI 277 LILILOPO
VISEGESE WILAYA YA KISARAWE**

Tafadhali husika na mada tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ilipokea maombi ya Ardhi ya kampuni tajwa hapo juu kwa ajili ya uwekezaji wa Kiwanda cha kemikali za nitro.
3. Halmashauri ya Wilaya imeyashughulikia maombi hayo na kwa sasa yapo kwenye hatua za utwaaji wa ardhi. Utambuzi wa ardhi (Demarcation) yenye ukubwa wa ekari 277 umefanyika, zoezi la uthamini **uwandani pamoja** uhakiki (Disclosure) kwa wananchi 116 katika eneo hilo umefanyika, aidha mwekezaji amehakikishia serikali (Commitment letter) kuwa atalipa fidia kwa mali za wananchi hao waliobainishwa katika eneo hilo.
4. Shughuli zinazoendelea kwa sasa ni ukamilishaji wa taarifa ya uthamini ili iidhinishwe na kulipa fidia, Usajili wa upimaji wa eneo hilo (Survey) na baadaye maombi ya hati (Derivative right Of Occupancy) yatawasilishwa kwako kwa ajili ya mwekezaji huyu.
5. Pamoja na barua hii, Ofisi inamtambulisha mwekezaji huyu kwa hatua zozote ambazo ofisi yako itaona zinafaa kwa wakati huu ambapo halmashauri inaendelea kusimamia hatua zilizobaki katika kukamilisha utwaaji wa ardhi hiyo.
6. Naomba kuwasilisha kwa hatua zako.


Jumanne S. Mwampashi
K.n.y Mkurugenzi Mtendaji (W)
KISARAWE

Nakala: Mkurugenzi
Kampuni ya Ideal Detonators Tanzania
14111 Street Masaki Road, Tour Drive
S.L.P 2860
DAR ES SALAAM

The District Executive Director's Office, P.O Box 28001 Kisarawe, 28 Bomani Road, 61401 Kisarawe, Coast Region. Phone: 023 2401045, Fax: 023 2401046, www.kisarawedc.go.tz, Email: ded.kisarawe@pwani.go.tz

MKI/Emc